


# Tufundishane



TOLEO LA 12, JULAI 2020



## Mbinu za Vikundi Katika Darasa Lenye Wanafunzi Wengi.

### 2. Mwalimu wa Digitali

*Ufundishaji na mabadiliko ya teknolojia*

### 6. Mwalimu Mkuu

*Nafasi yake katika kuelekea mafanikio  
ya Ufundishaji na Ujifunzaji*

# Moyo wa Mwalimu

Wengine huja wakitabasamu, wengine kwa macho ya machozi. Wengine wakiwa wamelowa jasho kwa kutembea umbali mrefu kati ya nyumbani na shule, wengine huja wakiwa wamejikunyata kwenye viunga nje ya darasa wakitetemeka kutohana na bardi. Jambo moja huwafanya wote kuwa sawa ni sare zao walizovaa.

Kengele ya asubuhi inalia na hukimbilia kwenye madarasa yao, wakichukua vitabu vyao na vifaa vingine vya kujifunzia na kuviweka tayari kwa kujifunza kama vile ndio tumaini lao la mwisho. Makumi au mamia yao huelekea kwenye madawati yao, wakichukua viti kabla ya mwalimu kuingia darasani.

Mwalimu huingia akitabasamu na baada tu ya kusema, "Habari za asubuhi wanafunzi ..." watoto kwa pamoja hujibu na kuitikia kwa kutabasamu, na hivyo kusababisha hali ambayo inafanya kufundisha na kujifunza vyema.

Jambo moja la kweli, wanafunzi wote wanaweza wakawa wamevaa sare na kufanya kufanana lakini hutoka mazingira mbalimbali. Watoto wengine hutoka kwenye familia tofauti tofauti wengine katika familia ya mzazi mmoja; wengine katika familia ya baba na mama, wengine katika familia kubwa; wengine kutoka familia zilizunjika na wengine ni yatima. Inahitaji kuwa zaidi ya mwalimu kuelewa wanafunzi hawa kwani hakuna njia moja na mfanano katika maisha.

Ukielewa mtoto mmoja mmoja, basi utajua jinsi ya kuwasaidia shida zao katika kujifunza na tabia zao. Inachukua jukumu la mwalimu kuwa kama mzazi ili kuweza kufanikisha malezi bora. Hatufundishi tu kwa madhumuni ya kielimu au taaluma, lakini pia tunatoa maarifa mapana kusaidia wanafunzi wetu kuwajibika zaidi, na kuishi maisha yanayokubalika katika jamii kadiri wanavyokua. Kama mzazi anavyolea na kuwatanza watoto wao, sisi waalimu tunalo jukumu hilo pia. Jukumu la malezi na makuzi linapaswa kuwa msingi wa kazi na taaluma yetu.

Kama mwalimu, wewe ni mfanano wa kuigwa, mzazi wa pili na mwongozo kwa maisha yote ya wanafunzi wako. Watoto ni kama saruji iliyo mbichi; ambayo huweza kuwekwa alama kwa kila kitu ambacho wamefundishwa. Kwa hivyo, walimu wanapaswa kuwa na uhusiano zaidi ya ule wa kitaaluma ili kuhamasisha



wanafunzi kuelekea katika ukuaji bora na hatimaye kufurahi katika kujifunza masomo yao.

Je, Kwako! Kufundisha ni kazi inayolipa bili au ni maisha yako kwa ujumla? Kama mzazi wa pili, fanya kazi katika kujenga akili na maadili ya watoto, kuwasaidia kutambua talanta zao na kufikia malengo yao.

Wanafunzi hutumia wakati au muda mwingi shulenii kuliko nyumbani, kwa hivyo tunahitaji kuwafanya wahisi kuwa wako salama vya kutosha. Hatimaye, watakuwa makini zaidi katika masomo yao na watawaheshimu walimu wao kwa kuonyesha tabia na nidhamu bora.

Mwalimu anapaswa kumwona mwanafunzi kama rafiki na kuwa mmoja kama wao. Mara tu mwanafunzi anapohisi kuwa mwalimu anathamini na kutambua jinsi mwanafunzi anavyojihisi yeye kama mwanafunzi, wanafunzi wanahisi wako kwenye ukurasa mmoja na waalimu wao na kwa kweli watamuamini mwalimu wao zaidi.

Tunapaswa kutoa mwongozo zaidi kuliko kuhukumu, kukosoa au hata kuwapa majina mabaya watoto. Hii huwafanya wajisikie salama, na hata kuwageuza wale wasiofaa zaidi kuwa washiriki wazuri darasani.

Mwalimu mwenye furaha hufanya wanafunzi wenyewe furaha ambaa huleta mazingira ya kufundisha na kujifunza kuwa mazingira salama na kufanya kila siku kuwa ya furaha kwa kila mwanafunzi!



# Mwalimu Wa Digitali

Na Mwl. Abdul Mdee, Mkuu wa Shule ya Msingi Usa, Wilaya ya Meru-Arusha.

**N**apenda kuchukua fursa hii ya pekee kusema machache kuhusu mabadiliko ya karne ya 21 na umuhimu wa sisi kama walimu kubadilika ili kuendana na madiliko hayo na kuleta tija katika ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wetu.


Ni ukweli usiofichika kwamba tupo katika karne ya 21 na kumekuwa na mabadiliko makubwa ya kitekinolojia na mabadiliko haya kutufikisha katika zama mpya ya habari na mawasiliano au ulimwengu wa kiditali- "*The Information Age*". Katika zama hizi tumeshuhudia mapinduzi ya kidijiti ambayo hufanya hata sisi wenyewe kuona kuwa kuna utofauti mkubwa sana kati ya mwaka hadi mwaka mwingine. Madiliko haya hutuonyesha utofauti mkubwa kati ya ulimwengu tulio kua sisi tukiwa watoto na ulimwengu ambao wanafunzi wetu wanakuwa sasa. Mfano mzuri katika hili ni upatikaji wa habari na taarifa kwa sasa nitofauti sana na hapo zamani. Tunashudia leo jinsi gani taarifa au habari zinavyopatikana na kusambaa kwa urahisi na haraka tofauti na hapo awali.

Utofauti kati ya ulimwengu tuliokuwa sisi kama watoto na ulimwengu wa sasa, unatutaka sisi kama walimu pia kubadilika kwa namna tofauti tofauti. Kwa mujibu wa kazi yetu ya ufundishaji tunahitajika kubadilika kuendana na uhitaji wa wanafunzi au mtoto wa sasa. Kwani ni dhahiri kwamba jinsi ulivyojifunza wewe wakati ukiwa darasa la kwanza sio sawa na mtoto waleo wa

darasa la kwanza anapaswa kujifunza. Kwani kati ka ulimwengu wa sasa tumeona utofauti mkubwa katika maswala kama vile intaneti, simu janja, bishara za mitandaoni, mitando ya kijamii kama vile WhatsApp, tweeter, maktaba za mtandaoni, nakadhalika.

Kulingana na mabadiliko haya, tuhitaji mwanafunzi ambaye huweza kufikiri kwa kina, kudadisi na kuhoji mambo kwa mtazamo tofauti tofauti, mwanafunzi ambaye anaweza kufanya mawasiliano vyema, kushirikiana na mwenye ubunifu katika kutatua changamoto mbalimbali zinazotuzunguka. Hatuwezi kufanikiwa tusipo badilika hususan kwa sisi walimu katika kujifunza ili kujijengea uwezo wa kutosha katika ufundishaji wetu kwa ujumla.


Hivyo tunaona dhahiri kwamba siwezi kufundisha kwa namna ileile ambaye mimi nilifundishwa miaka kumi au miaka ishirini iliyo pita. Ili kuweza kuhakikisha wanafunzi wangu wanafanikiwa kitaaluma na kimaisha nilazima kufundisha kulingana na uhitaji na mabadiliko ya ulimwengu wa sasa. Swali ni kwamba, sisi kama walimu tumewezaje au tunatumiaje fursa za mapinduzi haya ya kidijiti katika kujijengea maarifa na ujuzi mpya na hatimaye kuboresha ufundishaji wetu na ujifunzaji wa wanafunzi? Je, wajua kuwa kuna maarifa na ujuzi mwingi unaweza kujipatia kwa sasa kupitia mapinduzi ya kidijiti?



Walimu wengi tumezoea kupatiwa mafunzo ya moja kwa moja yaani warsha kama njia ya kutujengea uwezo wa kufanya vizuri zaidi katika kazi yetu ya ufundishaji. Ni kweli kabisa serikali ya Tanzania na wahisani mbalimbali wa elimu wamekuwa mstari wa mbele katika kuhakisha walimu tunawezo wa kutosha na kutupatia warsha na rasilimali mbalimbali. Lakini katika ulimwengu huu wa sasa wa mapinduzi ya habari na mawasiliano unaweza wewe mwenyewe kuamua unavyotaka kwa kupitia nyenzo na fursa mbalimbali za kimtandao.

Unaweza kuamua kuwa mwalimu mahiri kwa kujiongezea maarifa na kutumia rasilimali mbalimbali zilopo katika tovuti na sehemu mbalimbali za mtandaoni kukuza umahiri wako na hatimae kuboresha ufundishaji na matokeo ya ujifunzaji kwa wanafunzi wetu.

Tofauti na hapo zamani, leo uzoefu wangu unanionyesha kwamba kuna idadi kubwa ya walimu ambao humiliiki *smartphones* (*simu janja*). Pia kulingana na tafiti mbalimbali zilizofanyika kusini mwa bara la Afrika inasemekana zaidi ya watu milioni 250 wanatumia simu za mkononi na walimu wakiwemo. Hivyo mimi kama mwalimu ninapenda kutoa wito kwa walimu wenzangu kutumia nyenzo hii ya pekee ambayo inaweza kutunganisha na kuturuhusu kupata maarifa na ujuzi mpya, mbinu, mikakati, zana na rasilimali mbalimbali kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika madarasa yetu. Sambamba na hili tunaweza kutumia applications mbalimbali kama vile google, youtube, websites za kieleimu, na kadhalika katika kujipatia maarifa na ujuzi na hatimae kufundishia kwa ufanisi zaidi. Hatuwezi kuhakikisha tunakua katika kada yetu ya ualimu lakini pia kuwa fundisha vyema watoto kwa kutegemea pekee mafunzo ya warsha na kitabu cha kiada cha darasani.



# Mbinu za Vikundi Katika Darasa Lenye Wanafunzi Wengi

**M**ara nyingi walimu tunapata changamoto kubwa sana ya kutumia mbinu shirikishi kwa kusema kuwa tuna wanafunzi wengi darasani kuliko kawaida. Kulingana na changamoto hii walimu wengi tumejikita katika ufundishaji ambao haumzingatii mwanafunzi. Licha ya changamoto hii bado yatupasa kuhakikisha kuwa wanafunzi wetu wanashiriki somo kikamilifu kwa kadiri iwezekanavyo ili waweze kujifunza kwa umahiri unaotakiwa katika kila somo. Kwa msingi huo ninapenda kutumia fursa hii kuonyesha jinsi gani mwalimu anawenza kutumia kazi za makundi kama moja kati ya mbinu shirikishi za kufundishia na kujifunza. Pia kupitia mfano wa andalio la somo, tunaweza kujifunza zaidi jinsi gani ya kutumia mbinu ya kazi za makundi darasani.

Kazi za vikundi ni mbinu ya majadiliano baina ya mwanafunzi na mwanafunzi. Mbinu hii ambayo ni shirikishi na huhusisha zaidi ubongo kuliko zile nyingine ambazo hazimzingatii mwanafunzi. Hivyo kazi ya vikundi inafaidisha wanafunzi wenzi, hata kama wanafunzi wachache wanakuwa nije ya kazi. Katika kazi ya vikundi, wanafunzi wenye uwezo wa juu wanapata fursa ya kufundisha wanafunzi wenye uwezo wa chini, ambao wakati mwingine hufanikiwa zaidi kuliko mwalimu anapofundisha. Hatimaye, kazi ya vikundi hutoa fursa kwa wanafunzi kujifunza ujuzi halisi au stadi za maisha kama vile ushirikiano na mawasiliano, ambayo ni muhimu katika ulimwengu halisi.

Katika kazi za vikundi kuna mambo kadha wa kadha ya tupasa kuyazingaitia:

- i) Uundaji wa makundi,
- ii) Shughuli za vikundi,
- iii) Majukumu ya Mwalimu na
- iv) Majukumu ya mwanafunzi.

**i)Uundaji wa makundi:** Ili mbinu hii iweze kufanikisha ujifunzaji wa wanafunzi kwa ufanisi wa hali ya juu ni vyema mwalimu ukazingatia mambo yafuatayo. *Baadhi ya vigezo ni kama vile: Idadi ya wanafunzi katika kila kundi.* Inapendekezwa kwamba kuwe na idadi chache ya wanafunzi katika kila kundi kulingana na idadi ya jumla ya wanafunzi wako katika darasa. Kufanya hivyo utatoa nafasi ya kila mwanafunzi kushiriki kikamilifu na kujifunza vyema. Pia uundaji wa makundi uzingatie uwezo tofauti tofauti wa wanafunzi yaani kuwe kunamchanganyiko wa wanafunzi wenye uwezo mkubwa wa kati na wale ambao uwezo wao upo chini. Bila kusahau uwepo wa jinsia tofauti tofauti katika kila kundi. Hii hutoa fursa ya kila mwanafunzi kujifunza kutoka kwa mwanafunzi mwingine.

**ii)Shunguli za vikundi:** Jambo jingine la kuzingatia ni kazi au shughuli ambazo kila kundi litaptiwa kufanya. Ni vizuri kuwa na kazi za makundi kabla ya kuingia darasani kadhalika kazi hizo ziwe zinamaelekezo yanayojitosheleza. Kabla ya wanafunzi kukaa kwenye makundi yao ni vyema wakafahamu jambo au kazi wanayo tarajiwa kufanya. Pia inashauriwa kila kundi liwe lina kazi tofauti na kundi lingine kwa kufanya hivyo utaepuka kurudia jambo moja mara kwa mara kadhalika wanafunzi hawata poteza mwitikio wakati wa uwasilishaji na kuwezesha kila mwanafunzi na kikundi kujifunza kutoka kwa kundi lingine. Muda wa wanafunzi kufanya kazi hizo za makundi ni lazima uzingatiwe na uwe na uhalisia na kila kikundi waweze kujua ni muda gani watatumia kufanya kazi yao.

**iii) Majukumu ya mwalimu:** Jukumu la mwalimu ni kutayarisha mazingira yafaayo kwa ujifunzaji wa mada,mazingira ambayo wanafunzi wale wataingiliana na kuwasiliana. Mazingira ambayo mwalimu mwenyewe atajizuia au kusema yale wanafunzi wake wanaweza kufanya au kusema. Mwalimu anatakiwa kuandaa shughuli za vikundi na kuhakikisha kila kiongozi wa kikundi anapati-kana. *Kusimamia muda wakati shughuli za vikundi zikiendelea.* Vilevile mwalimu anatakiwa kuzungukia kikundi kimoja baada ya kingine kuona kazi zinavyotendeka na kama kuna mahali penye shida kusaidia kundi. Mwalimu anapaswa kuwahimiza wanafunzi kujitegemea wao kwa wao hivyo wanapaswa kushirikiana badala ya kushindana. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuongoza wanafunzi kwa kueleza tu na wanafunzi ndio hufanya shughuli dasanasi.

Pia mwalimu huondoa tofauti mionganini mwa wanafunzi na kusaidia wanafunzi walemavu na kubuni mikakati ya kuhakikisha ubora wa ujifunzaji katika vikundi. Hali ambayo huchangia ushiriki wa wanafunzi wote na kuweza kuwajibika katika shughuli za kundi lao. Wanafunzi walemavu wana nafasi ya kushiriki na kukuza stadi kama vile kuzungumza. Mara baada ya vikundi kumaliza kazi zao, toa nafasi ya vikundi kuwasilisha walichojifunza na kutoa ufanuzi kwa kifupi.

**iv) Majukumu ya mwanafunzi:** Kutambua majukumu ya mwanafunzi katika kazi za vikundi hutuwezesha kujua kama wanafunzi wanafanya yale yawapasayo na kujifunza vyema. Kila mwanafunzi anapaswa kushiriki katika kutoa mazwazo yake kwa kundi, kuheshimu mawazo ya mtu mwingine, kuwasilisha yaliyo jadiliwa kwa wengine na kuchukua nukuu.



# Mwalimu Mkuu

*Nafasi yake kuelekea Mafanikio katika Ufundishaji na Ujifunzaji.*

**U**ongozi na usimamizi bora wa shule unamchang'o mkubwa sana kwa mafanikio ya mwanafunzi mmoja mmoja na kwa shule kwa ujumla. Uongozi bora katika shule ni jambo la msingi sana hasa nyakati zetu hizi. Makala hii itaangazia nafaasi ya mwalimu mkuu katika kusimamia mafanikio ya shule katika ufundishaji na ujifunzaji. Tafiti zinaonesha kuwa mafanikio ya taasisi yoyote yanategemea kwa kiasi kikubwa ufanisi wa mifumo ya uongozi na usimamizi wake.

## ***Nafasi ya Mwalimu Mkuu kama Msimamizi***

Mafanikio ya shule yoyote hutegemea ufanisi wa mwalimu mkuu katika usimamizi wake. Hapa kwetu Tanzania waalimu wakuu huteuliwa kuto-ka mionganoni mwa walimu waliopo kazini. Ndio kusema walimu wote wanapaswa kujua na kujenga umahiri katika uongozi. Mwalimu anapoteuliwa kuwa mwalimu mkuu anajikuta ghafla katika wajibu tofauti, majukumu tofauti, changamoto tofauti, kujitoa kwa upya nakadhalika.

Hata hivyo mwalimu mkuu analogukumu la kuyaweka wazi malengo ya shule kwa kila mdau na kuhakikisha kuwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, rasilimali fedha kwa matumizi ya shule vinapatikana pamoja na kuwatia moyo waalimu, wanafunzi na wazazi ili kuleta uhai ndani ya shule na kuboresha utendaji kazi. Ndio kusema kuwa mwalimu mkuuu anawajibika kaatika Nyanja kadhaa ambazo anatakiwa wajibike kwazo.

## ***Mwalimu Mkuu na Mwajiri wake***

Mwalimu Mkuu anawajibika kwa mwajiri wake. Waajiri wanategemea ubora wa kazi, uaminifu na uadilifu. Haya ni mambo matatu ambayo yakizin-gatiwa yatamsaidia kujenga mahusiano mazuri na mwajiri wake na hivyo kuchangia katika mafanikio yake kama kiongozi na msimazi wa shule kwa ujumla. Ndio kusema, mwalimu mkuu ajitahidi kukwepa vishawishi vya kutumia vibaya mamlaka na majukumu waliyopewa na waajiri wao.

## ***Mwalimu Mkuu na taluma ya Ualimu***

Taaluma ya ualimu ina maadili na miiko yake. Mwalimu mkuu kama walimu wengine, ni lazima awe mfano katika kuzingatia maadili ya kazi ya ualimu. Kwa kuheshimu nafasi yao, kuna

sehemu na maeneo ya mkusanyiko ya kijamii am-bayo hawategemewi kuonekana! Kuna namna ya lugha na misemo ambayo hawapaswi kuchangamana nayo, ipo mitindo ya mavazi ambayo taluma yao haiwaruhusu kuva! Haya ni baadhi tu ya mambo ambayo mwalimu mkuu anaalikwa kuwa mfano wa kuigwa na waalimu wengine.

## ***Mwalimu Mkuu na jamii inayomzunguka***

Shule zetu sio visiwa – ni sehemu ya jamii. Mwalimu mkuu anapaswa kuijua vema jamii inayomzungu-ka na kujenga nayo mahusiano mazuri. Kwa njia hii atawea kuwafanya wanajamii kuvutiwa na kinachoendelea shulenii hasa kuhusiana na elimu ya watoto wao. Elimu wanayopata wanafunzi shulenii ni lazima iakisi maisha ya kawaida kwenye jamii zao. Ilenge kuboresha hali ya maisha kwenye jamii. Mwalimu Mkuu achagize matumizi ya elimu inayotolewa shulenii iboreshe mifumo ya maisha ndani ya jamii. Kwa mfano dhana ya usafi wa mwili na mazingira, maadili mema, kilimo cha bustani za mboga mboga n.k zidhiihirike katika maisha ya jamii wanayotoka wanafunzi.

## ***Mwalimu Mkuu na Walimu wenzake***

Ubora na weledi wa mwalimu mkuu kama kiongozi unahitajika sana katika mahusiano yake na waalimu wenzake ili kufikia malengo mahususi ya shule kama taasisi na kwa namna ya pekee malengo ya ufundishaji na ujifunzaji. Katika kuwasimamia walimu wenzake kwa ufanisi, mwalimu mkuu anapaswa kufikiri na kuzingatia mambo kadhaa ya msingi:

- **Heshima:** Awe mstari wa mbele na mfano bora wa kuigwa kwa kujiheshimu na kuwasheshimu wengine na kuwaamini anaowaongoza na jamii inayomzunguka kwa ujumla.
- **Haki:** Awe mtu wa haki na usawa. Asioneshe upendeleo kwa baadhi ya walimu, wafanya-kazi au wanafunzi. Hili linaweza kusababisha kutokuelewana na kufifisha ufanisi kama timu yenye malengo mamoja.
- **Kutunza Siri:** Anapaswa kuheshimu na kutunza siri za walimu/wafanyakazi wengine anazojua kutokana na utendaji wake wa kila siku. Ajitahidi asiwajadili/kuwasema kwa wengine kwani wakijua watajisikia vibaya na akakosa uaminifu (trust).

- **Kiungo:** Awaunganishe walimu wenzake watembee pamoja katika kufikia malengo ya shule. Uongozi bora unahusisha uwezo wa kuwaunganisha walimu wote na kuwa kitu ki-moja kwa manufaa ya shule na katika kufikia malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.
- **Maadili na Weledi:** Aoneshe juhudzi za maku-sudi za kukuza maadili na weledi kwa wafanya-kazi wote. Maadili mema kama niliviyotangulia kusema ni tunu msingi kwa kada ya ualimu.
- **Kukaimisha Majukumu:** Aweze kuwaamini waalimu wenzake na kukaimisha (delegate) baadhi ya majukumu kwa waalimu wengine kadiri ya uwezo, uzoefu na viwango vyao vya uaminifu. Akumbuke daima kuwa yeze ndiye atakaye wajibika hivyo awe makini katika ku-kaimisha majukumu na madaraka yake.
- **Uongozi Shirikishi:** Ajaribu sana kuwashiriki-sha walimu wenzake kabla hajafanya maamuzi makubwa ya kikazi yatakayowahusu aidha kama watekelezaji wake au wasimamizi wa te-kelezaji wa maamuzi hayo.
- **Mawasiliano:** Zaidi ya yote ajitahidi kuboresha mfumo wa mawasiliano katika shule yake. Tafiti zinaonesha kuwa mawasiliano mazuri (effec-tive communication) ni kama moyo wa tasisi yoyote. Ajenge mfumo mzuri wa mawasiliano utakaowezesha wadau kupata taarifa muhimu kwa wakati pamoja na kutoa mrejesho (feed-back) kwa wakati. Mawasiliano hafifu, yasiyoz-ingatia muda (time frames) yamekuwa sababu ya utendaji mbaya na ufanisi hafifu kwa wa-alimu wakuu wengi na kwa uongozi wa taasisi kwa ujumla.

Kwa kuhitimisha, inafaa sana waalimu wakuu wajue na kuzingatia kuwa wao sio waalimu wakuu kwa ajili yao! Cheo chao ni dhamana na wana-alikwa kukitumia kuwahudumia wanaowaongoza na kamwe isiwe ni fursa ya kujinufaisha binafsi bali nafasi ya kuwaongoza waalimu katika kufikia malengo ya elimu bora kwa wanafunzi wao, am-bao kimsingi ndio kiini cha uwepo wa shule na na-fasi zao.

#### **Rejea:**

- Bakda, S. (2004). Management and Evaluation of Schools. Nairobi. Oxford University Press, East Africa Ltd
- Conlow, R. (2005). Excellence in Supervision: Essential Skills for New Supervisor. New Delhi. Crisp Publications Inc
- Mbiti, D.M. (2009). Foundations for School Administra-tion. Nairobi. Oxford University Press, East Africa Ltd



# Najivunia kuwa Mwalimu

## ***Ualimu ualimu! Upo kwenye damu yangu.***

Niliupenda tangu nikiwa mdogo, darasa la sita tuseme. Mwalimu wangu wa hisabati alinifanya nipayende ualimu kwa jinsi alivyokua anafundisha kwa juhudhi, huku akijitahidi kutumia mbinu zinazomsaidia mwanafunzi aelewe haraka na apende somo hilo, ambalo watu wengi wanalihofia.

Ni miaka 14 sasa, nafundisha masomo ya kuhesabu, kusoma na kuandika darasa la pili. Naipenda sana kazi yangu, maana nafundisha ila pia mara nyingine nafundishwa na najifunza mengi kila siku yanayohusu kazi yangu ya ualimu.

Napenda nikushirikishe vitu viwili muhimu ambavyo nimevivuna katika hii kazi na ningependa walimu wengine wajifunze.

Hivi vitu vimenisaidia ndani na nje ya darasa katika maisha ninayoishi na jamii ilionizunguka.

## **Cha kwanza kabisa ni Kujiamini**

Silaha muhimu ya mwalimu ni kujiamini. Ualimu umenijengea haiba ya kujiamini kwa vile darasani mimi ndo naongoza njia kwa wanafunzi wangu kupata maarifa na kuwajengea mazingira ya uhuru kuwa wabunifu ili wawe na uelewa wa kina zaidi hasa katika zama hizi za tekinolojia, karne ya 21.

Nimejifunza kwamba mavazi yana mchango mkubwa kumjengea mtu kujiamini na kuaminika katika jamii. Mavazi ya haiba yanajenga heshima kati ya mwalimu na wanafunzi wake, kitu ambacho kinachangia kujenga kujiamini kwa kiasi kikubwa.

Kupitia kujiamini, mwalimu anakua na unyumbulifu wa kutumia mbinu mbali mbali akiwa anafundisha. Hii inasaidia sana kujali wanafunzi wenye tofauti katika uelewa pamoja na wale wenye mahitaji maalum ya kujifunza.

Kwa upande wa jamii, ualimu umenisaidia kuwa na uwezo wa kujiamini hasa pale ninapoongea mbele za watu. Kama mwanamke, nimekua mfano kwa wengi hasa pale ninapokua na ujasiri wa kuzungumza na watu ata wawe wengi kiasi gani, kwa ufasaha kabisa.

## **Cha pili ni Ushirikiano**

Darasani, tunashirikiana na wanafunzi katika swala zima la kujifunza. Kwa mfano, nandaa somo

au mada kuzingatia azimio la kazi, huku nikiwapa wanafunzi wangu kipaumbele maana wao ndio watendaji wakuu katika swala zima la ujifunzaji.

Hii inamsaidia sana mwanafunzi kukumbuka alichojifunza na alichofundishwa.

Pia, nawapa wanafunzi nafasi ya kutengeneza zana ili kuwajengea ubunifu na kutunza kumbukumbu na tabia ya kushirikiana vizuri na wanafunzi wengine

Napenda sana kutumia mbinu shirikishi darasani. Siku moja, nilikua darasani nikagundua kuna mwanafunzi mmoja hashiriki ipasavyo. Alikua analala darasani kama anaumwa, basi nikachukua jukumu kumhoji mara baada ya kipindi.

Alinieleza mambo mengi yanayomsumbu mpaka kumkosesha utulivu darasani. Alikua na njaa, hana daftari, kalamu, begi wala nguo za shule.

Nilichukua jukumu la kumuita mzazi ili nithibitishe ukweli wa mwanafunzi. Mzazi wake alithibitisha kwamba ni kweli kama alivyoeleza mtoto, maana maisha ni magumu sana ila hivyo hivyo anajitahidi hata wale mlo mmoja kwa siku.

Binafsi nilisikitika sana, nilimshirikisha mwalimu mwenzangu akamletea begi, na mimi nikamnunulia daftari, kalamu na penseli pamoja na kumpatia chakula cha mchana.

Sasahivi, anafurahia sana kuja shule.

Kwa upande wa jamii, ualimu umenisaidia kutumia saikolojia yangu kuishi na watu kwa upendo na amani. Kushirikiana na wengine katika jamii ni swala muhimu sana, ikiwemo kwenye matukio ya shida na raha.


Binadamu tunategemeana, hakuna aliyekamilika. Najivunia uwezo nilionao kuishi kwenye mazingira ambayo kuna watu wa aina tofauti na kuweza kuishi nao huku nikijenga na kuimarisha umoja ndani ya jamii hiyo.

Kupitia izo nguzo mbili, nilifanikiwa kupata tuzo ya "Teacher of Distinction Award," (Tuzo ya mwalimu mahiri) tarehe 06.07.2018 ambayo ili-tolewa Arusha City Council Education Office.

Napenda ualimu, najivunia kuwa mwalimu pia napenda kujifunza kila siku Maishani mwangu.

***Imeandikwa na Mwl. Neema Godwin Mtenga***

# Ulinzi na Usalama wa Mtoto



**S**wala la ulinzi na usalama wa mtoto limepamba moto sana katika miaka michache iliyopita. Hivi sasa, maswala yanayohusu ulinzi na usalama wa mtoto yamekuwa kipaumbele sana katika mashirika mbalimbali kitaifa na hata kimataifa. Mimi na wewe tunaweza kujiuliza ni kwanini sasa na sio miaka minge ya nyuma iliyopita:

Ni Dhahiri kwamba hivi karibuni kumekuwa na matukio mbali mbali yanayoonyesha ukatili juu ya watoto. Mengi tunayasikia katika vyombo vya habari, lakini pia mengine tunayaona yakinkeka katika jamii zetu.

Watoto wote wana haki ya kulindwa, kila mtoto ana haki ya kuishi, kuwa salama, kuwa na wazazi/walezi, kusikilizwa, kupata huduma muhimu na kukuwa katika mazingira yaliyo salama.

Chanzo cha ulinzi wa mtoto ni familia. Wazazi na walezi wana jukumu la kuhakikisha kuwa watoto wapo katika mazingira yaliyo salama. Ni jukumu letu kutengeneza mazingira yaliyo salama na rafiki kwa mtoto aidha nyumbani au nje ya nyumbani.

*Je, kipindi hichi cha likizo ya lazima ambacho Watoto wamekua nyumbani kwa sababu ya ugonjwa wa Korona, ni namna gani ulimlinda/unamlinda mtoto wako?*

Kila siku watoto wanakabiliwa na ukatili, unyanyasaji, unyonyaji, ubaguzi, utelekezwaji na utengwaji.

**Je, unyanyasaji wa mtoto ni nini?**

Unyanyasaji wa mtoto ni uvunjaji wa sheria kuhusu haki za mtoto kunakopelekea athari za kimwili, kimaadili au kihisia ikiwemo vipigo, kutu-

kanwa matusi, kubaguliwa, kutojaliwa unyanyasaji wa kingono na utumikishwaji.

**Kuna aina kuu nne za unyanyasaji**

1. *Unyanyasaji wa kimwili*- Huu ni unyanyasaji unaoothiri mwili kwa ujumla, kama vile kupigwa makofi, ngumi, kuchapwa, kuchomwa na pasi, kuchomwa na kisu cha moto, kusukumwa, kutikiswa.

2. *Unyanyasaji wa Kisaikolojia/Kihisia*- Unyanyasaji huu unaathiri hisia na akili ya mtoto. Kwa mfano: kutukanwa, kufokewa, kusingiziwa, kuaibishwa, kudhalilishwa, kutishiwa yaani vitemdo vya ishara kama vile kumshikia mtoto panga ukimwambia nitakupiga au kukukatakata.

3. *Unyanyasaji wa kingono*- Ni Unyanyasaji unaomuumiza mtoto kijinsia/kingono. Mfano wa unyanyasaji huu ni kubakwa, kulawitiwa, kukeketwa au kushikwa sehemu za mwili.

4. *Kutelekezwa*- Ni Kutojaliwa na wazazi au walezi. kwa mfano mtoto kukaa siku nzima bila kupewa chakula.

Mara nyingi, athari za unyanyasaji huingiliana, Mtoto aliyenyanyaswa kimwili, kwa mfano mara nyingi anayanyasika kihisia na mtoto aliye nyanyaswa kingono pia anaweza kutojaliwa, kuumia kihisia na kuathirika kisaikolojia.

Unyanyasaji unaathari kubwa sana kwa mtoto. Kwa hali ya muonekano wa nje tu unaweza kumouna mtoto na michubuko na makovu ya vichapo, au madhara makubwa kama kuvunjika, kutokwa damu au hata kifo. Dalili za kutelekezwa tunazowenza kuona ni kama vile afya duni na kudumaa,

na matatatizo ya ukuwaji wa ubongo. Lakini pia kuna zile athari tusizosiona kwa macho, yani athari za kisaikolojia; madhara ya hapo kwa hapo yaani utotoni yanaweza kuwa hofu, kutokujiamini au kuamini watu wengine, sonona, kutokuwa na uwezo wa kudhibiti mkojo (incontinence). Madhara haya pia huonekana ukubwani kwa mfano hali ya kutaka kujua, kujingiza kwenye madawa ya kulevyia ili kupooza akili, kujikataa, udkozi au wizi (kleptomania), kuwa na shauku (anxiety), wasiwasi na/ msongo au mshtuko baada ya kurejea tukio flani (Trauma).

Inatupasa tukumbuke yakuwa, siyo watu wa nje ya familia tu wanaonyanyassa Watoto. Katika Matukio mengi ya hivi karibuni tumesikia aidha Mama mzazi anamkatakata mtoto, Baba mzazi kumlawiti mtoto, visa vya mwalimu kubaka mwanafunzi; hivyo ni jukumu la kila mmoja wetu kusimama katika nafasi yake kama mwana jamii kuwaepusha Watoto na vitendo vya kikatili, kuwalinda na kuripoti pale tunapohitaji msaada wa vyombo vya kiserikali.



## Ualimu Kazi Yangu

**M**imi ni mwalimu Sarah William. Nilajiriwa mwaka 2003 baada ya kufanya kazi shule binafsi kwa miaka mitatu, kutokana na ajira za serikali kwa kipindi hicho kukosekana. Niliolewa mwaka 2001, lakini mume wangu alifariki mwaka 2005 na sijaolewa tena mpaka sasa. Nilijaliwa kupata mtoto mmoja ambaye kwa sasa anasoma kidato cha nne

Kazi yangu ya ualimu imenisaidia sana, niliachwa kwenye chumba kimoja lakini mpaka sasa, nimeweza kununua kiwanja na kujenga nyumba mbili ambazo moja ninapangisha na nyingine nashi mwenywewe.

Kupitia kazi ya ualimu, nimeweza pia kununua usafiri binafsi. Kazi ya ualimu imekua mtaji mkubwa sana kwangu. Pia nafanya shughuli za kilimo hii imenisaidia kuboresha maisha yangu kufanana na wafanyakazi wa sekta mbalimbali za ajira.

Naheshimika sana kwa wanaume na wana-wake wenzangu kutokana na juhudzi zangu pamoja na changamoto za maisha. Kazi ya ualimu haina mshahara mkubwa lakini imenifundisha mengi ikiwemo kuweza kubana matumizi ili kuweza kuendana na uchumi

Kupitia kazi ya ualimu, mtu anaweza kufiika mbali sana, na kuishi kama mfano wa kuigwa na jamii iliomzunguka.

*By; Sarah W. Mritha*



**Je, Unataka kusikika katika toleo letu Jipy?**  
**Tunataka kusikia kutoka kwako!**

Kama shule yako inayo habari au jambo lolote ambalo mnajivunia na kutaka kwashirikisha walimu wengine ili waweze kunufaika katika swala zima la ufundishaji na ujifunzaji, tutumie ili tuweze kuchapisha katika toleo letu la Tufundishane kwa awamu inayofuata.

Tunakaribisha makala mbalimbali yanayo zungumzia ufundishaji mzu-ri na usimamizi bora wa shule. Pia tunakaribisha kazi za sanaa mfano mashairi kutoka kwa walimu na wanafunzi.



Physical Address  
2<sup>nd</sup> Floor, King Solomon's House  
Anglican Church Compound  
Old Moshi Road  
Arusha - Tanzania

[www.thefoundationfortomorrow.org](http://www.thefoundationfortomorrow.org)  
[info@thefoundationfortomorrow.org](mailto:info@thefoundationfortomorrow.org)  
Facebook@TheFoundationForTommorrow  
Twitter@TFFTAFRICA

For comments or Suggestions  
[noah@thefoundationfortomorrow.org](mailto:noah@thefoundationfortomorrow.org)  
+255 753 661 770